

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Habari na Uhushiano
S.L.P 76959
Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA

SHIRIKA LA RELI TANZANIA KUREJESHA SAFARI ZA TRENI KATI YA DAR ES SALAAM NA MOSHI NDANI YA SIKU 14

Dar es Salaam, Juni 04, 2020.

Shirika la Reli Tanzania – TRC linatarajia kurejesha safari za treni za mizigo na abiria kati ya Dar es Salaam na Moshi mkoani Kilimanjaro ndani ya siku 14 kufuatia kusitishwa kwa huduma za usafiri wa treni kutokana na mafuriko yaliyosabishwa na mto Pangani kujaa baada ya mvua zilizonyesha katika maeneo ya mkoa wa Kilimanjaro na nchi jirani ya Kenya hivi karibuni Mei 2020.

Mafuriko hayo yamesababisha uharibifu wa miundombinu ya reli kati ya Stesheni ya Buiko na Hedaru ambapo kipande cha Reli chenye urefu wa Kilometra 1.6 kilifunikwa na maji kwa zaidi ya siku 21.

Kutokana na hali hiyo Shirika la Reli lilisitisha kwa muda safari za treni za abiria na mizigo kati ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Kilimanjaro kuanzia tarehe 10 mwezi Mei 2020 ambapo baadaye Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alifanya ziara katika eneo hilo akiambatana na timu ya wataalamu kutoka TRC ili kuona maendeleo ya utengenezaji wa njia hiyo.

Aidha, kutokana na tathmini iliyofanywa na wataalamu kutoka TRC kukamilisha utengenezaji na kurejesha njia hiyo katika hali ya usalama na hatimaye safari za treni kuelekea Moshi kuanza tena, Shirika linaendelea na kazi ya kuinua tuta la reli kati ya Stesheni ya Buiko na Hedaru ambapo matengezo yanatarajiwaa kukamilika ndani ya siku 14 tangu kuanza kwa kazi hiyo tarehe 1, Juni 2020.

Shirika linaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Jamila Mbarouk'.

Jamila Mbarouk
Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhushiano TRC